LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
3rd Episode: Internet
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS:
Anchor for: Intro / Autro
Bibiy............Main Character.
Rossie..........(Same character)
Alma...........(Same character)
Internet cafe Attendant/Muhudumu........A man (young adult.)
Kibegu.......A Teenage boy...16 yrs.
Timo.........A teenage boy.....15 yrs.
Debate Conductor...........Woman (Adult).

Intro:
Hujambo na karibu kwenye mfululizo wa mchezo wa hadithi katika makala haya ya Jifunze kwa Kusikiliza ambapo tunaangazia maswala mbalimbali yanayo wakabili wasichana. Leo hii wasichana wanajifunza mengi kuhusu mtandao wa internet na jinsi mtandao huo unavyoweza kuwasaidia. Bibiy na marafiki zake wanapata fursa ya kuunda kikundi chao cha Girl Power ambacho lengo lake hasa ni kuwahimiza wasichana kutimiza malengo yao. Bibiy na wenzake leo hii wanautumia mtandao wa internet kutafiti juu ya mada watakayo watakayoitetea kwenye mjadala. Karibu msikilizaji ,kwenye sehemu ya tatu kaika mfululizo wa makala ya Jifunze kwa Kusikiliza kwa jina Mtandao wa Internet:

SCENE ONE:

Sign Tune
(Bibiy na marafiki zake wako mjini wanaelekea kwenye internet cafe.....kelele za magari na watu zinasikika .)
BIBIY: Haa! Jamani mnaonaje mambo yalivyo mazuri. Angalau tumetimiza lengo letu mjini ndio hapa tumefika..nakumbuka nyanya yangu aliwahi kunihadithia hadithi juu ya kisa cha mbuzi kubakia na mkia mfupi..aliniambia ni kwa

sababu mbuzi alikuwa kila mara anakwenda kinyume na wanyama wenzake, alikuwa hafuati kule wanyama wenzake walikokuwa wakielekea. Wakati wanyama walipokuwa wanjitahidi kuelekea upande wa kufaulu maishani yeye mbuzi alikwenda kwengine kabisa. Nyana aliniambia kuwa wakati huo wanyama walipewa mikia mirefu kutokana na bidii yao ya kuamka mapema ili kuwahi nafasi ya mbele katika msitari kule kwenye uwanja wa kupewa alama za mafanikio. Basi aliniambia kila mara mnyama aliongezewa alama ya maendeleo kutoakna na urefu wa mkia wake lakini masikini mbuzi hakupata bahati hiyo ng'o. (Wasichana wanacheka )......

ALMA: Aah Bibiy! Mimi hata siwezi kukubali kuwa kama mbuzi hata kidogo..Loo! niwe na mkia mfupi..hiyo haitawezekana kamwe..sitaki mimi niwe na mkia mfupi kama mbuzi? No way! (anapasua kicheko)

BIBIY: Ndio maana marafiki zangu sisi sote tusikubali kumfuata mbuzi tusije tukabakia na mikia mifupi inatubidi tuyafuate maendeleo yaliko kama wale wanyama wengine werevu. Nafikiria ni muhimu kwetu sisi kujifunza namna ya kuitumia tarakilishi yaani computer na hasa mtandao wa internet kwa kuwa tutapata faida kubwa kielimu au mnasemaje wenzangu? Kikundi Chetu cha Girl Power lazima kiwe kielelezo cha kuwapa moyo wasichana wenzetu ili nao wajitahidi kufikia malengo yao kwa kuutumia mtandao wa internet katika computer hiyo ni muhimu.

ROSSIE: Unayosema ni kweli Bibiy nafikiria wazo la sisi kuwa ni kielelezo kwa wasichana wengine ni zuri kabisa..Sisi tuwe waanzilishi na wasichana wengine watuige.

BIBIY: Hasa! Rossie umegonga msumari kichwani. Nasisi tunaweza tu kufanikiwa iwapo tutashirikiana vyema..umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Tukishirikiana tunaweza kuwa kielelezo chema kwa wasichana wengine na pia tunaweza kuwaelekeza wasichana wenzetu mambo ya kufanya.

Unapokuwa kielelezo kizuri inakubidi utoe mfano bora wa kuigwa.

ALMA: Jamani hebu ngojeni kwanza.ngojeni dakika moja tu!..wacheni stori zote kwanza hebu angalieni nguo hii mbona nzuri kweli kweli , wow! mnaionaje ilivyo nzuri yaani hii nguo ni poa kweli au sio?

ROSSIE: Loo! Ni nzuri kweli tena inapendeza. Kwanza hizo rangi zake ni poa kweli. Bibiy nguo hiyo inaweza kukupendeza sana na hiyo style yako ya nywele pamoja na figa yako ..utapendeza sana.

ALMA: Unajua Bibiy anayoyasema Rossie ni ya kweli kabisa. Wewe ni mrembo hadi kila mtu huwa anakuzungumza..tena hata siendi mbali hebu geuka ungalie kule nyuma waangalie wale vijana pale bila shaka wananong'ona juu yako!

ROSSIE: Aah wee waache tu wakaange mbuyu hadi wenyewe wachoke watanong’ona mpaka mate yawakauke ukweli ni kwamba Bibiy wewe ni mrembo bwana.. rafiki yangu you are beautiful. Hakuna atakeweza kujilinganisha na urembo wako.wewe ni bomba kichizi!

BIBIY: Jamani Rossie basi nashukuru kwa sifa ulizonipamba, asante kwa ukarimu wako.... Shhhhh! OK, basi mazunumzo yaishe kwani tumeshafika kwenye internet cafe. Tuingieni ndani ili tukapate maelezo zaidi.
Music............

SCENE TWO:
ATTENDANT: Hello! Wasichana hamjambo na karibuni sana je naweza kuwasaidia?

BIBIY: Hatujambo! ndio unaweza kutusaidia tunahitaji kutumia mtandao wa internet.

ATTENDAT: Well, kutumia computer au internet hasa kwa

shughuli za shule au mkitaka kufanya homework au pengine mnataka kuzungumza na marafiki yaani kuchat...basi mnahitaji mtu mwenye ujuzi kuwaongoza ili mfikie yale mnayoyatafuta katika mtandao na wakati huo huo mtaalamu huyo atawafahamisha pia hatari zilizomo katika mtandao.

ALMA: Lakini kwa nini mpaka tupate mtu wa kutuongoza mbona mimi najua kutumia computer? Sidhani kama tunahitaji mtu wa kutusaidia.

ATTENDANT: Ni kweli lakini kujua kuitumia computer ni jambo moja na kujua kuutumia vyema mtandao wa internet ni jambo jingine tofauti kwa kuwa internet ni ulimwengu mkubwa wa kipekee na hivyo basi mnahitaji maelekezo. Mnahitaji kuelekezwa ili mpate kuzijua website za wasichana wa marika yenu ambazo zitawanufaisha. Kwa mfano website inayotowa maelekezo ya utendaji bora katika somo la hisababti ambayo nafikiri ni muhimu kwa kazi zenu za shule na masomo yenu kwa jumla au pia kuna websites ambazo zinatoa maelezo ya jinsi utakavyo weza kuvinjari nafasi za masomo ya juu na kadhalika. Kwa kweli mkijua hasa namna ya kuutumia mtandao wa internet mtaweza kuwa na nafasi nzuri ya kuandaa maisha yenu ya usoni au kuona jinsi wanafunzi wa marika kama yenu haya mnavyoweza kujiandalia mambo mazuri ya usoni.

ROSSIE: Wow! Hiyo ni habari njema. Sasa naona kweli tunahitaji kujifunza kama vile Bibiy alivyosema kuwa tunahitaji kujifunza jinsi ya kuitumia computer na pia mtandao wa internet kwa kuwa vitu hivi ni muhimu sana kwenye maisha yetu.

BIBIY: Ndio maana mie nasisitiza juu ya kuanzisha kikundi chetu cha Girl Power halafu tuwe na tovuti yetu pia.Inatubidi tunoe ujuzi wetu kwa kujifunza mengi kupitia vyanzo mbalimbali katika internet baada ya kufanya utafiti.

ATTENDANT: Naam wasichana nataka pia mjue kuwa mtandao wa internet ni mahala pazuri pa kuanzia safari yenu hiyo. Na katika mtandao mnaweza pia kufaidika na taarifa nyingi tu

zinazo wahusu nyie vijana katika Nyanja mbali mbali kama vile elimu, afya, uhusiano na mengine mengi sana ndio maana mimi niko hapa kwa ajili ya kutoa usaidizi kwenu nataka kuwapa vidokezo vya namna ya kuzifikia tovuti hizo kwa urahisi.

ALMA: Samahani naomba kuuliza.. ulitaja juu ya hatari katika mtandao je hatari hiyo ni ipi? una maana computer inaweza kunilipukia usoni kwa ghafla ama?

ATTENDANT: Hapana..hapana ninamaanisha kuwa lazima muwe na ujuzi wa kuitumia internet kwa njia salama na kuhakikisha kuwa mnafuata sheria zilizowekwa kwa mfano mnatakikana mjue kuwa watu mnaokutana nao online yaani kwenye mtandao hao watabakia kuwa wageni kwenu wakati wote kwa hivyo hamtapanga kukutana na watu hao bila ya ruhusa ya wazazi wenu au bila ya kuwafahimsha wazazi wenu. Na pia lazima mkumbuke kila wakati kuhifadhi taarifa zenu za kibinafsi kwa mfano hamruhusiwi kuwasilisha habari zozote kuwahusu kama vile wewe ni msichana au mvulana, anuani zenu za email na pia si vyema wala haikubaliki kutumia lugha ya matusi au vitisho kwenye mtandao.

BIBIY: OK, mnasikia hayo wenzangu hapa tunawajibika kufuata sheria kama ilivyo desturi yetu na pia lazima tuwe waangalifu na urafiki wa online,pili hamna cha kuapa hovyo hovyo, hamna kuchokozana na wala mazungumzo machafu hayaruhusiwi kabisa..yaani tunahitaji kuendeleza hali shwari na hilo hasa ndilo lengo letu.

ATTENDANT: Na jingine ambalo ni la muhimu ni kuhusu muda mtakao tumia kwenye computer..mimi ningewashuri kuwa msipende sana kutumia muda mrefu kwenye computer hatutaki muifanyishe kazi sana mikono yenu na vidole vyenu vidogo na pia kuyaumiza macho yenu kwani viungo hivyo muhimu katika mwili wa binadamu vinahitaji mapumziko.

ALMA: Cool, mara moja tu kwa wiki katika internet cafe inatutosha na pia bora kwa mifuko yetu.

ATTENDANT: Sawa basi kama mpo tayari nadhani tutaweza kufungua akaunti yenu ya e-mail ya kikundi. Na sijui mnataka kutafiti nini leo?

BIBIY: wajua tunataka kushiriki kwenye mjadala na mada yenyewe inahuhsu ukeketaji yaani “je ukeketaji uachwe uendelee au upigwe vita?". Katika mada hii wavulana wanaunga mkono ukeketaji na sisi wasichana tunapinga ndio maana tunataka kufanya utafiti wa kutosha ili tukawatoe jasho wavulana..

ATTENDANT: Oh, ni mada moto kweli, hadi siku za hivi karibuni mada hiyo ilikuwa ni mwiko kuijadili hadharani lakini nina hakika mtashinda kwani mtajiandaa vilivyo kukabiliana na wavulana.

BIBIY: Lengo letu ni kupambana na vitendo vya ukeketaji kwa sababu wasichana wanaendelea kuteseka na wengine wanapoteza maisha yao.

DRUMS

SCENE THREE:
(Sauti za watu zinasikika)
DEBATE CONDUCTOR: mabibi na mabwana leo tumeshuhudia mada nyeti ya ukeketaji na ambayo imefanyiwa utafiti wa kutosha. Pande zote mbili zimeonyesha umahiri mkubwa bila shaka mtakubakliana name kuwa mawasiliano ni jambo muhimu katika maisha. Na kabla ya kufikia ukingoni ya mjadala huu nawaita tenea washiriki kutoka pande zote mbili ili kukamilisha mada kabla ya kumteuwa mshindi kwa hiyo ntamuita Kibegu kwanza aje ate kuwa ukeketaji uachwe uendelee.
(Makofi....)

KIBEGU: Asante sana mwenyekiti, mabibi na mabwana kwa mara nyingine tena nasimama mbele yenu kuzungumza kwa nguvu zangu zote nikiunga mkono kuwa Ukeketaji undelee kwa

sababu shughuli hii imekuwepo kwa karne nyingi zilizopita katika jamii yetu na hii ni kwa ajili ya hekima ya mababu zetu ambao waliona kuwa bila ya ukeketaji wanawake wangekuwa na tamaa nyingi, pili ukeketaji unaongeza urembo wa wanawake na pia ukeketaji unawsaidia wanawake kuepukana na maradhi mengi kama msisimuko wa damu na shida nyingi za kiakili namalizia kwa kusema ikiwa wanaume lazima wafanyiwe tohara kwa ajili ya kulinda usafi na afya kwa nini wanawake wasifanyiwe hivyo. Wenzangu kupinga FGM ni sawa na kuendeleza harakati za wananwake ambazo hazina kichwa wala miguu. Asanteni.
(Makofi)

DEBATE CONDUCTOR: Asante Kibegu kwa mchango wako zamu ni yako sasa Rossie.

ROSSIE: asante sana mwenyekiti mabibi na mabwana na wanafunzi wenzangu. Napinga kwa sauti kubwa sababu zilizotolewa na upande wa wapinzani. Ijapokuwa ukeketaji au FGM bado unaendelea katika nchi nyingi barani Afrika na sehemu zingine ulimwenguni ningependa kusisitiza kuwa shughuli hii inakiuka haki za binadamu za mtoto wa kike na mwanamke ni lazima tuungane pamoja, kuupiga vita ukeketaji kwani ni kitendo cha kinyama. Asanteni.
(Makofi).

DEBATE CONDUCTOR: Na sasa namuita Timo akamilishe mada kwa upande wa kikosi chake juu ya FGM.

TIMO: Asante bibi mwenyekiti. Yote ya muhimu kuhusu mada ya leo tumekwisha yasema na langu sasa ni kufikisha ujumbe kwa kusema sisi sote kwa pamoja tuunge mkono kuwa ukeketaji undelee daima kwani hii ndio njia ya pekee ya kuzuia maambukizi ya virusi vya HIV na ugonjwa wa Ukimwi. Asanteni.
(Makofi)

DEBATE CONDUCTOR: Namkaribisha sasa msemaji wetu wa mwisho nae ni, Alma.

ALMA: Mabibi na mabwana pamoja na wanafunzi wenzangu kabla sijazungumza zaidi napenda kuwauliza swali wapinzani wetu Je ni vipi ukeketaji dhidi ya wasichana wasiokuwa na hatia utakavyo kinga maambukizi ya virusi vya HIV na ugonjwa wa Ukimwi?
(Makofi) Kuwaumiza wanawake kwenye sehemu zao za siri bila sababu zozote za kitalaamu kunasababisha maumivu makali na pia hali hiyo inachangia athari za muda mrefu za kiafya hii ikiwa ni pamoja na matatizo wakati wa kujifungua na pia hatari kwa mtoto atakayezaliwa .FGM inaathiri miili ya wasichana na wanawake . Kwa maelezo hayo natumai nimewashawishi wapinzani wetu vya kutosha. Kwa niaba ya wenzangu nawashauri wapinzani wetu wavuke sakafu na kuungana nasi katika harakati za kupinga ukeketaji dhidi ya wasichana na wanawake.
(Makofi).

AFRICAN DRUMS

DEBATE CONDUCTOR: Mabibi na mabwana mambo yote mmeyasikia na sasa umefika wakati wa kutoa uamuzi nao wa wazee wa baraza wameamua hivi.. (watu wananog’ona kwa sauti zinazosikika).

DEBATE CONDUCTOR: Kimya tafadhali naomba tukae kimya!. OK, asanteni... na washindi wa mjadala wetu wa leo ni.. (kimya) – upande wa wasichana!
(Makofi.)

MUSIC

BIBIY: Hongereni sana wenzangu! Huu ni wakati wa furaha kubwa katika maisha yangu. Mmefanya kazi nzuri sana yaani mada mmeijadili kwa ufasaha na umahiri mkubwa.

ALMA: Asante Bibiy ushindi huu ni kwa ajili ya kujiamini tunashukuru kikundi chetu cha Girl Power.

ROSSIE: Yaani hata siamini kwa kweli tumewaonyesha waichana wenzetu mfano mwema nafikiri mfano huu tuuendeleze hadi darasani tuwaonyeshe wavulana kuwa hata nasi tunaweza kufanya yale wanayoyaweza yaani tuko sawa kiakili na kiuwezo.

BIBIY: Kilichonifurahisha zaidi ni uwezo wetu wa kuitumia computer kukusanya habari. Kwa kweli computer imegeuka kuwa chombo chenye nguvu kilichotufanya tuwashinde wavulana. Sasa basi wenzangu msisahau kuwa tutakwenda tena kwenye internet café wiki ijayo.

MUSIC

Autro: Na mpaka hapo ndio tumekamilisha sehemu ya tatu ya mchezo wa hadithi kwa jina Mtandao wa Internet. Bibiy na wenzake wamepata ushindi mkubwa dhidi ya wavulana katika mada waliyoifanyia utafiti kwenye mtandao wa internet. Makala haya ya Jifunze kwa Kusikiliza yanaangazia mada mbalimbali zinazowakabili wasichana. Iwapo unataka kusikiliza mchezo huu au pia kumwambia rafiki asikilize tembelea tovuti yetu HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe . Usikose kujiunga nasi wiki ijayo ambapo Bibiy anawasaidia wasichana wenzake kupambana na kudhalilishwa kingono. Hadi tutakapokutana tena kwaheri.

END